FUNZO LA 40

1. Je, Sauli alipokataa kumtii Mungu, Mungu alimchagua nani awe mfalme wa pili?
-Daudi.

2. Je, tofauti kati ya Daudi na Sauli ilikuwa gani?
-Sauli hakuamini kuwa alizaliwa katika dhambi na kutengana na Mungu, ila Daudi aliamini.
-Sauli hakuamini kuwa Mungu huadhibu dhambi yote kwa kifo, Daudi aliamini.
-Sauli hakuamini kuwa ni Mungu pekee ndiye aliyeweza kumuokoa, Daudi aliamini.
.
3. Je, baada ya Daudi kumaliza kujenga nyumba yake, alitaka kufanya nini?
-Daudi alitaka kumjengea Mungu nyumba.

4. Je, ni nani aliyestahili kumjengea Mungu nyumba?
-Mwana wa Daudi, Sulemani.

5. Je, ahadi kubwa ambayo Mungu alimuahidi Daudi ilikuwa gani?
-Mungu alimuahidi kuwa atatuma Mwokozi kupitia uzao wa Daudi.

6. Je, hekalu aliyomjengea Mungu Sulemani ilifananaje na hema ambayo Waisraeli walimjengea Mungu jangwani?
-Hema ya Mungu na hekalu zilikuwa na chumba cha kwanza kilichoitwa Chumba Kitakatifu.



-Hema ya Mungu na hekalu zilikuwa na chumba cha pili kilichoitwa Chumba Kitakatifu Zaidi.
-Hema ya Mungu na hekalu zilikuwa na pazia ambayo ilitenganisha hivyo vyumba viwili.

7. Je, kwa sababu Mungu ni mtakatifu na anachukia dhambi yote, kuhani mkuu alifanya nini katika Chumba Kitakatifu Zaidi?
-Alinyunyuza damu ya mnyama juu ya Sanduku la Agano.

8. Je, Mungu alifanya nini alipoona damu aliyonyunyuza kuhani mkuu juu ya Sanduku la Agano?
-Mungu alizuia adhabu ya dhambi kwa watu kwa mwaka mmoja hadi siku ambayo malipo bora ya dhambi yatakapofanywa.

9. Je, ni kwa nini damu ya mnyama haikuweza kulipia dhambi za watu?
-Kwa sababu dhambi lazima ilipwe kwa kifo cha mwenye dhambi.

10. Baada ya Sulemani kufa, nini kilichowafanyikia Waisraeli?
-Waisraeli hawakukubaliana nani awe mfalme anayefuata.

11. Je, makabila kumi ya kaskazini yaliitwaje?
-Israeli.

12. Je, makabila mawili ya kusini yaliitwaje?
-Yuda.

-Je, kwa nini Mungu hunena na watu mara kwa mara?
-Ili waokolewe.

-Mungu pia amewapa watu ujumbe wake ili wawaambie wengine ili waokolewe.

-Mungu alimpa Nuhu ujumbe wake ili awaambie watu ili waokolewe.

-Mungu alimpa Musa ujumbe wake ili awaabie Farao na Wamisri, ili waokolewe.

-Mungu alimpa Yoshua ujumbe wake ili awaabie Waisraeli, ili waokolewe.

-Siku moja, Mungu alimuita Muisraeli mmoja aitwaye Yona.

-Mungu alimpa Yona ujumbe wake na kumwamuru apeleke ujumbe wake kwa watu waovu waliokuwa wakiishi kwa mji uliokuwa ukiitwa Ninawi.

-Watu waliokuwa wakiishi katika mji wa Ninawi waliitwa Waasiri.

Tusome Yona 1:1-3a

1-Basi neno la Bwana lilimjia Yona, mwana wa Amitai,
kusema,
2-Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukapige
kelele juu yake; kwa maana uovu wao umepanda juu mbele



zangu.
3-Lakini Yona akaondoka akimbilie Tarshishi, apate
kujiepusha na uso wa Bwana;

-Je, kwa nini Mungu alimtaka Yona aende Ninawi?

-Kwa sababu Mungu aliwapenda watu wa Ninawi.

-Kwa sababu Mungu alitaka kuwaokoa watu wa Ninawi kutoka kwa nguvu za dhambi, kifo na Shetani.

-Je, kwa nini Yona alitoroka?

-Yona alitoroka kwa sababu hakutaka kwenda kwa mji wa Ninawi.

-Je, kwa nini Yona hakutaka kwenda kwa mji wa Ninawi?

-Kwa sababu watu wa Ninawi walikuwa waovu sana.
-Kwa sababu watu wa Ninawi walikuwa adui wa Israeli.

-Kwa sababu Yona hakutaka Mungu awaokoe watu wa Ninawi.

-Je, Yona aliweza kutoroka kutoka kwa Mungu?

Tusome Yona 1:3b-10

3-Akatelemka hata Yafa, akaona merikebu inayokwenda
Tarshishi; basi, akatoa nauli, akapanda merikebuni, aende
pamoja nao Tarshishi, ajiepushe na uso wa Bwana.

4-Lakini Bwana alituma upepo mkuu baharini, ikawa tufani kubwa baharini, hata merikebu ikawa karibu na kuvunjika.

5-Basi wale mabaharia wakaogopa, kila mtu akamwomba mungu wake; nao wakatupa baharini shehena iliyokuwa merikebuni, ili kuupunguza uzito wake. Lakini Yona alikuwa ameshuka hata pande za ndani za merikebu; akajilaza, akapata usingizi.

6-Basi nahodha akamwendea, akamwambia, Una nini, Ewe ulalaye usingizi? Amka, ukamwombe Mungu wako; labda Mungu huyo atatukumbuka, tusipotee.

7-Wakasemezana kila mtu na mwenzake, Haya, na mpige kura, mpate kujua mabaya haya yametupata kwa sababu ya nani. Basi wakapiga kura, nayo kura ikamwangukia Yona.

8-Ndipo wakamwambia, Tafadhali utuambie, wewe ambaye mabaya haya yametupata kwa sababu yako; kazi yako ni kazi gani? Nawe umetoka wapi? Nchi yako ni nchi ipi? Nawe u mtu wa kabila gani?

9-Akawaambia, Mimi ni Mwebrania; nami namcha Bwana, Mungu wa mbingu, aliyeziumba bahari na nchi kavu.

10-Ndipo watu wale wakaogopa mno, wakamwambia, Ni jambo gani hili ulilolitenda! Kwa maana watu wale walijua ya kuwa amekimbia, ajiepushe na uso wa Bwana, kwa sababu alikuwa amewajulisha.

-Je, Yona aliweza kutoroka kutoka kwa Mungu?
-La.

-Je, Yona aliweza kujificha kutoka kwa Mungu?
-La.



-Je, Yona aliweza kuepuka Mungu?
-La.

-Hakuna anayeweza kuepukana na Mungu.

-Hata Shetani na mapepo wake hawawezi kuepukana na Mungu.

Tusome Yona 1:11-17

11-Basi wakamwambia, Tukutende nini, ili bahari itulie? Kwa maana bahari ilikuwa inazidi kuchafuka.

12-Naye akawaambia, Nikamateni, mnitupe baharini; basi bahari itatulia; kwa maana najua ya kuwa ni kwa ajili yangu tufani hii imewapata.

13-Lakini wale watu wakavuta makasia kwa nguvu, ili wapate kurudi pwani, wasiweze; kwa maana bahari ilizidi kuwachafukia sana.

14-Basi wakamlilia Bwana, wakasema, Twakuomba, Ee Bwana, twakuomba, tusiangamie kwa ajili ya uhai wa mtu huyu, wala usitupatilize kwa ajili ya damu isiyo na hatia; kwa maana wewe, Bwana, umefanya kama ulivyopenda.

15-Basi wakamkamata Yona, wakamtupa baharini, nayo bahari ikaacha kuchafuka.

16-Ndipo wale watu wakamwogopa Bwana mno, wakamtolea Bwana sadaka, na kuweka nadhiri.

17-Bwana akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku.

-Je, Mungu alifanya nini Yona alipokataa kumtii kwa kukataa kwenda Ninawi?

-Mungu alituma samaki mkubwa akammeza Yona.

-Je, Yona alikaa siku ngapi tumboni mwa samaki?
-Siku tatu mchana na usiku.

-Je, Yona aliweza kujiokoa katika tumbo la yule samaki mkubwa?
-La.

-Je, ni nani aliyeweza kumuokoa Yona?
-Mungu.

-Je, watu wote wanafananaje na Yona?

-Kama vile Yona hakuweza kujiokoa katika tumbo la yule samaki mkubwa.

-Watu wote hawawezi kujiokoa kutoka kwa nguvu za dhambi kifo na Shetani.

-Kama vile ni Mungu pekee aliyeweza kumuokoa Yona, ni Mungu pekee anayeweza kuwaokoa watu wote.

-Je, Yona alifanya nini tumboni mwa yule samaki mkubwa?

Tusome Yona 2:1



1-Ndipo Yona akamwomba Bwana, Mungu wake, katika tumbo la yule samaki,

-Yona alikubali kuwa hakumtii Mungu.
-Yona alikubali kuwa alitenda dhambi dhidi ya Mungu.

-Yona alimuita Mungu amuokoe.

-Je, Mungu alimuokoa Yona?

Tusome Yona 2:10

10-Bwana akasema na yule samaki, naye akamtapika Yona pwani.

-Je, Mungu alifanya nini Yona alipokubali kuwa hakumtii Munga na alitenda dhambi dhidi ya Mungu?

-Mungu alimfanya yule samaki mkubwa kumtapika Yona katika nchi kavu.

-Je, kwa nini Mungu alimuokoa Yona?

-Kwa sababu Yona alikubali kuwa hakumtii Mungu.

-Kwa sababu Yona alikubali kuwa alitenda dhambi dhidi ya Mungu.

-Je, baada ya Mungu kumuokoa Yona, alimwambia kuwa si lazima aende Ninawi?

-La.

Tusome Yona 3:1-2

1-Neno la Bwana likamjia Yona mara ya pili, kusema,
2-Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa; ukaihubiri habari nitakayokuamuru.

-Mungu habadiliki.

-Mungu kamwe habadiliki.

-Mungu bado alimtaka Yona awapelekee watu wa Ninawi ujumbe wake.

-Mungu bado alitaka kuwaokoa watu wa Ninawi.

-Je sasa, Yona alimtii Mungu na kwenda Ninawi?

Tusome Yona 3:3-5 & 10

3-Basi Yona akaondoka, akaenda Ninawi, kama Bwana alivyonena. Basi Ninawi ulikuwa mji mkubwa mno, ukubwa wake mwendo wa siku tatu.
4-Yona akaanza kuuingia mji mwendo wa siku moja, akapaza sauti yake, akasema, Baada ya siku arobaini Ninawi utaangamizwa.
5-Basi watu wa Ninawi wakamsadiki Mungu; wakatangaza kufunga, wakajivika nguo za magunia, tangu yeye aliye mkubwa hata aliye mdogo.



10-Mungu akaona matendo yao, ya kuwa wameiacha njia yao mbaya. Basi Mungu akalighairi neno lile baya, ambalo alisema atawatenda; asilitende.

-Sasa, Yona alimtii Mungu na kwenda Ninawi.
-Sasa, Yona alipeleka ujumbe wa Mungu Ninawi.

-Yona aliwaambia watu wa Ninawi waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Je, watu wa Ninawi walisikiliza ujumbe wa Mungu ambao Yona aliwaambia?
-Ndiyo.

-Mungu anakutaka uwe kama watu wa Ninawi.

-Mungu anakutaka usikilize ujumbe wake kama watu wa Ninawi.

-Mungu anakutaka uamini ujumbe wake kama watu wa Ninawi.

-Mungu anakutaka uache njia ya dhambi na ufuate njia ya Mungu.

-Mungu pia aliwachagua watu wengi wawe wajumbe wake wa kueneza ujumbe wake.

-Je, watu ambao Mungu aliwachagua wawe wajumbe wake wa kuwaambia watu ujumbe wake, waliitwaje?
-Manabii.

-Mungu aliwatuma baadhi ya manabii kwa makabila kumi ya Israeli.

-Mungu alituma baadhi ya manabii kwa makabila mawili ya Yuda.

-Je, manabii waliwaambia nini watu?
-Waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Manabii waliwaambia watu pia kuwa Mungu aliwataka waharibu mifano yao.

-Mmoja wa manabii aliitwa Isaya.
-Nabii Isaya alienda kwa makabila kumi ya Israeli.

-Kifuatacho ndicho Mungu alichowaambia Waisraeli kupitia kwa Isaya:

Tusome Isaya 10:6

6-Nitamtuma juu ya taifa lenye kukufuru, nitampa maagizo juu ya watu wa ghadhabu yangu, ateke nyara, na kuchukua mateka, na kuwakanyaga kama matope ya njiani.

-Je, nini kingewafanyikia makabila kumi ya Israeli iwapo hawangeacha njia ya dhambi na kufuata njia ya Mungu?

-Mungu angewatuma Waasiri wayashinde makabila kumi ya Israeli na kuwachukua kuwa watumwa wao.



-Nabii mwingine wa Mungu aliitwa Yeremia.

-Nabii Yeremia alienda kwa makabila mawili ya Yuda.

-Kifuatacho ndicho Mungu alichowaambia Yuda kupitia kwa Yeremia:

Tusome Yeremia 20:5

5-Tena mali zote za mji huu, na mapato yake yote, na vitu vyake vya thamani vyote pia, naam, hazina zote za wafalme wa Yuda, nitavitia katika mikono ya adui zao, watakaowateka nyara, na kuwakamata, na kuwachukua mpaka Babeli.

-Je, nini kingewafanyikia makabila mawili ya Yuda iwapo hawangeacha njia ya dhambi na kufuata njia ya Mungu?

-Mungu angewatuma Wababeli wayashinde makabila mawili ya Yuda na kuwachukua kuwa watumwa wao.

-Mungu hajabadilika.

-Mungu bado anataka watu waache njia ya dhambi na kufuata njia ya Mungu.

-Mungu atawaadhibu kwa kifo cha milele wale ambao hawataacha njia ya dhambi na kufuata njia ya Mungu.